JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI NOVEMBA, 2023

### 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2023 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka yalipata mvua za juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu wa mwezi Novemba. Hali hii ilisababisha mafuriko, ongezeko la unyevu ardhini, kina cha maji na malisho kwa baadhi ya maeneo. Hata hivyo, vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, kati mwa nchi, nyanda za juu kaskazini mashariki na nyanda za juu kusini magharibi. Hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2023 pamoja na mvua za Msimu, 2023/2024.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Novemba, 2023

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2023 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo mengi nchini. Aidha, maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ikihusisha pwani ya kaskazini, ukanda wa ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki, yalipata mvua za juu ya wastani. Vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi na kusababisha mafuriko, uharibifu wa miundombinu na mali, na kuathiri shughuli za kiuchumi. Mnamo tarehe 01 Novemba, 2023 kituo cha Lyamungu kilichopo mkoani Kilimanjaro kilipima milimita 185.0 za mvua kwa saa 24 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kwa mwezi Novemba, 2023 ikifuatiwa na Zanzibar (milimita 146.1) tarehe 5 Novemba na Tanga (milimita 134.0) mnamo tarehe 15 Novemba,2023. Jedwali 1 linaonyesha idadi ya siku ambazo vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi.

**Jedwali 1**. Idadi ya siku ambazo vipindi vya kubwa viliripotiwa vituoni kwa mwezi Novemba, 2023

| Kanda | Kituo | Siku | Mvua kubwa (mm) |
|---|---|---|---|
| **Pwani ya Kaskazini** | Tanga | 5 | ≥ 50 |
| | Handeni | 2 | ≥ 50 |
| | Pemba | 2 | ≥ 50 |
| | Zanzibar | 5 | ≥ 50 |
| | JNIA (Dar es Salaam) | 5 | ≥ 50 |
| | Kibaha | 2 | ≥ 50 |
| | Matangatuani | 7 | ≥ 50 |

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610


Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kizimbani | 5 | ≥ 50 |
| | Mlingano | 5 | ≥ 50 |
| | Dar Port | 2 | ≥ 50 |
| | Mahenge | 1 | ≥ 50 |
| **Nyanda za juu kaskazini mashariki** | Arusha | 1 | ≥ 50 |
| | KIA | 1 | ≥ 50 |
| | Moshi | 2 | ≥ 50 |
| | Lyamungu | 3 | ≥ 50 |
| | Babati | 1 | ≥ 50 |
| **Ukanda wa Ziwa Victoria** | Bukoba | 2 | ≥ 50 |
| | Musoma | 1 | ≥ 50 |
| | Mwanza | 2 | ≥ 50 |
| | Ukiriguru | 1 | ≥ 50 |
| **Kati** | Hombolo | 1 | ≥ 50 |
| **Nyanda za juu kusini magharibi** | Mbozi | 1 | ≥ 50 |

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2023 ukanda wa pwani ya kaskazini ulipata vipindi vingi vya mvua kubwa. Kituo cha Matangatuani kilichopo Pemba kilipata vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ndani ya saa 24 kwa siku saba. Aidha, vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 70 au zaidi ndani ya saa 24 ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 1.




**Kielelezo 2:** Vituo vilvyoripoti viwango vya mvua kubwa vya milimita 70 au zaidi ndani ya saa 24 kwa mwezi Novemba, 2023.

Ripoti kutoka katika vyombo vya habari zilithibitisha kutokea kwa athari katika baadhi ya mikoa ikiwemo mkoa wa Dar es Salaam baada ya mvua kubwa zilizopelekea mafuriko,

maji kuzunguka makazi na kuharibu mali, na kuathiri shughuli za kiuchumi baada ya kufungwa kwa barabara.



**Kielelezo 2**. Baadhi ya nyumba zilizopo pembezoni mwa bonde la Mto Msimbazi zikiwa zimezingirwa na maji baada ya mvua kubwa kunyesha usiku wa kuamkia tarehe 12 Novemba, 2023 (Source: Michuzi Blog).

### 1.2 Hali joto kwa mwezi Novemba, 2023

Katika kipindi cha mwezi Novemba 2023, hali ya joto ilijitokeza kwa baadhi ya maeneo nchini. Aidha, hakuna vipindi vya baridi kali au joto kali vilivyoripotiwa nchini. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 34.4 kilirikodiwa katika kituo cha Mpanda (mkoa wa Katavi) mnamo tarehe 1 Novemba, 2023 na kiwango cha chini zaidi cha nyuzi joto 11.0 °C kiliripotiwa katika kituo cha Igeri (Mkoa wa Njombe) mnamo tarehe 16 Novemba, 2023.

### 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Novemba, 2023

Katika kipindi cha mwezi Novemba, vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika maeneo machache nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mkoa wa Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba), maeneo ya kati mwa nchi (Singida na Dodoma), magharibi (Tabora), nyanda za juu kusini magharibi (Songwe) na nyanda za juu kaskazini mashariki (mkoa wa Arusha). Kasi na nguvu ya upepo ilisababisha athari mbalimbali. Athari hizo ni pamoja na ongezeko la vumbi, kupeperusha takataka na kusabisha kupungua kwa uono. Maeneo machache ya mwambao wa pwani yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa ya bahari na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika mwambao.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 14 Disemba, 2023*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz